JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

015

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 3 **Alhamisi, 14 Novemba 2019 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na tatu (13)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu C.
3. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (xv), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Ni kundi lipi kati ya yafuatayo linaonesha vyanzo muhimu vya kiuchumi katika Serikali ya Kiislamu?

A Al-ghanimah, Zaka, Al-ddiya, Al-kharaj, Al-fay, Al-Ushru na Sadaka.
B Sadaka, Zaka, Jizyah, Al-nafaqah, Al-fay, Al-ghanimah na Al-Ashru.
C Zaka, Sadaka, Al-kharaj, Al-Ja'alah, Al-fay, Al-ghanimah na Al-Ushru.
D Zaka, Sadaka, Fidya, Al-kharaj, Al-fay, Al-ghanimah na Al-Ushru.
E Zaka, Sadaka, Jizyah, Al-kharaj, Al-fay, Al-ghanimah na Al-Ushru.

(ii) Ni sababu ipi iliyofanya baadhi ya watu kuasi baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad (s.a.w)?

A Kukataa kutoa Zaka.
B Uroho wa madaraka.
C Ugumu wa sheria za Kiislamu.
D Kutompenda Khalifa Abubakar.
E Kukataa kupigana Jihad.

(iii) Kanuni ipi inatumika kuchuja Hadithi za Mtume (s.a.w)?

A Kuangalia urefu au ufupi wa Hadithi hiyo.
B Kuangalia sehemu iliyopokelewa Hadithi hiyo.
C Kuangalia wahusika waliomo kwenye Hadithi.
D Kuangalia maisha ya wapokezi wa Hadithi.
E Kuangalia matumizi ya Hadithi hiyo katika maisha.

(iv) Ikitokea msimulizi wa Hadithi anajulikana kuwa na uwezo mdogo wa kuhifadhi masimulizi, Hadithi yake itawekwa kwenye kundi lipi?

A Dhaifu
B Majuhul
C Maudhuu
D Marfuu
E Mursal

(v) "Ametuhadithia Abdallah bin Yusuf akasema: Ametupa habari Malik kutoka kwa Muhammad bin Ubair bin Mut'im kutoka kwa baba yake kwamba: wapokezi wote wa Hadithi hii ni wema na waadilifu." Hadithi hii inawekwa katika kundi lipi?

A Maudhuu
B Mursal
C Maqtuu
D Mutasil
E Sahih

(vi) Kwa kutumia mafunzo yatokanayo na Suratul-Fatiha, Muislamu anatakiwa kufanya nini kabla ya kuanza jambo lolote?

A Kusoma Audhubillahi Minashaitwanir Rajiim.
B Kusoma Bismillahir Rahmanir Rahim.
C Kusoma Subhana Rabia l-adhiimu.
D Kusoma lahaulawallakuwata ila billah.
E Kusoma fanaudhubillah min dhalika.

Scanned by CamScanner

(vii) Ni dhambi ipi kubwa iliyotajwa kwenye Suratul- Humazah?

A Kutukana. B Kusengenya. C Kuiba.
D Kupigana. E Kudanganya.

(viii) Bainisha tafsiri ya aya ya saba ya Suratul-Bayyina katika tafsiri zifuatazo:

A Ni mtume aliyetoka kwa Allah anayewasomea kurasa zilizotakaswa.
B Hakika wale walioamini na kutenda mema basi hao ndio wema wa viumbe.
C Ndani yake kuna sharia madhubuti.
D Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa).
E Kisha (nasema) sivyo hivyo, karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo).

(ix) Zifuatazo ni adabu za kusoma Qur'an tukufu **isipokuwa**:

A Kusoma ukiwa twahara na kuanza kwa kumlaani shetani.
B Kuanza kwa bismillahir na kuwa mnyenyekevu wakati wa kusoma.
C Kuanza kwa sauti ya chini kisha sauti ya juu wakati wa kusoma.
D Kusoma kwa sauti nzuri na kuzingatia maana ya kila aya.
E Kutekeleza maamrisho yake na kujizuia na makatazo yake.

(x) Ni kipengele kipi kati ya vifuatavyo kinachoonesha kazi kuu ya dini kwa mtazamo wa Uislamu?

A Kusimamia sheria za kumkomboa mwanadamu.
B Kuwakandamiza na kuwadhalilisha wanyonge.
C Kuwatawala watu katika nyanja kuu za maisha.
D Kuinyonya na kuidhulumu jamii.
E Kuwagawanya watu katika matabaka.

(xi) Kwa namna gani ndoa inamuhifadhi Muislamu na zinaa?

A Inamfanya aliyeoa asifikirie tendo la ndoa tena.
B Inasababisha kuwa na mwenza mmoja tu.
C Imeweka utaratibu madhubuti wa kukidhi haja.
D Inaepusha maharimu katika familia moja kuoana.
E Inawaweka wanandoa pamoja maisha yao yote.

(xii) Nini hukumu ya Mwanamke mjamzito aliyepewa talaka katika sheria ya Kiislamu?

A Eda ni miezi mitatu na siku kumi. B Eda ni miezi minne na siku kumi.
C Eda ni mwezi mmoja na siku kumi. D Eda hadi atakapomaliza kunyonyesha.
E Eda hadi pale atakapojifungua.

(xiii) Ni ipi adhabu ya mlevi katika sheria ya Kiislamu?

A Kuchapwa viboko mia moja.
B Kuchapwa viboko themanini.
C Kuchapwa viboko hamsini.
D Kuchapwa viboko arobaini.
E Kuchapwa viboko ishirini na moja.

Scanned by CamScanner

(xiv) Ipi ni maana sahihi ya kuamini siku ya mwisho?
A Unapokufa na kuoza ndio mwisho wa maisha.
B Kuna maisha ya milele baada ya kufufuliwa.
C Unapokufa nchi moja utafufuka nchi nyingine.
D Haiwezekani kufufuliwa tena baada ya kufa.
E Watu wema tu ndio watakaofufuliwa.

(xv) Jambo lipi lilisababisha ahitajike Mtume mwingine baada ya wa kwanza kurejea kwa mola wake?
A Mtume wa mwanzo alishindwa kupata wafuasi wengi.
B Mtume anayefuata alikuwa na mafundisho tofauti na aliyetangulia.
C Kulikuwepo taifa lililokaa muda mrefu bila ya Mtume.
D Mtume aliyetangulia alipelekwa kwa taifa maalum.
E Mtume aliyepelekwa mwanzo alikataliwa na watu wake.

2. Oanisha matendo ya Hija yaliyomo katika **Orodha A** na Majina ya matendo hayo yaliyomo **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A	**Orodha B**
(i) Mahujaji husimama, kuleta dhikri na kuomba dua mchana kutwa.	A Ifraad B Tamatui
(ii) Mahujaji hutia nia ya Hija na kuvaa Ihraam.	C Tawafu
(iii) Mahujaji hutembea mara saba baina ya Swafa na Marwa.	D Arafa
(iv) Hija iliyo nafuu kwa mahujaji wanaotoka mbali na Makka.	E Qiraan
(v) Mahujaji huzunguka Al-Kaaba mara saba kuanzia jiwe jeusi.	F Sai G Miiqat

SEHEMU B (Alama 35)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Fafanua kwa ufupi kwa nini mwanamke wa Kiislamu haruhusiwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja?

4. (a) Bainisha madhara matatu ya Riba.
(b) Toa hoja mbili jinsi gani utalipatia ufumbuzi tatizo la riba.

5. Tofautisha Qudra na Qadar ya Mwenyezi Mungu.

6. Bwana Juma na mkewe swaumu zao zilibatilika mchana wa mwezi wa Ramadhani. Orodhesha mambo matano yanayoweza kuwaharibia swaumu yao.

Scanned by CamScanner

7. Eleza hatua tano za kumkafini maiti wa kiume.

8. (a) Kwa nini Qur'an ilishushwa kidogo kidogo? Fafanua kwa kutoa sababu mbili.
   (b) Eleza njia kuu tatu zilizotumika kuhifadhiwa Qur-an.

9. Tofautisha vipengele vya Hadithi vifuatavyo:
   (a) Hadithi Qudusy na Hadithi Nabawiyyah
   (b) Aljar-hi na Ata-adili

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii.

10. Eleza mafunzo manne wanayoyapata Waislamu kuanzia kuumwa mpaka kutawafu kwa Mtume Muhammad (s.a.w).

11. Eleza namna Mtume (s.a.w) alivyoteremshiwa Qur'an kwa mara ya kwanza na kisha bainisha mafunzo manne yanayopaswa kufanyiwa kazi katika maisha ya kila siku kutokana na tukio hilo.

12. Eleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa Khutba ya Ijumaa.

13. Fafanua kazi tano za sheria ya Kiislamu katika jamii.

Scanned by CamScanner